

KCSE MOCKS

KISWAHILI PAPER 3

Consists 3 KCSE Mock set Exams.
(Class of KCSE March 2021)

For Marking Schemes Contact Mr Machuki
0795491185

Kenya Educators Contacts:

+254795491185

kenyaeducators@gmail.com

**For more e-learning resources contact Kenya
Educators via the contacts above.**

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0795491185

PRE-MOCK 1

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI

SAA 2 ½

JINA.....NAMBA YA MTAHINIWA.....

SAHIHI YA MTAHINIWA..... TAREHE.....KIDATO.....

MAAGIZO

Jibu maswali manne pekee.

Swali la kwanza ni la lazima

Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi Simulizi

Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
	Jumla 80	

LAZIMA SEHEMU YA A: TAMTHILIA P. Kea: Kigogo

1a. Mmesikia? Hamtatuletea wazimu wenu hapa! Nendeni kama mmekuja kutuhasimu.

i. Eleza muktadha wa maneno. (alama 4)

ii. Jadili umuhimu wa msemaji kwa hoja nne. (alama 4)

iii. Fafanua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)

b. Kenga alichangia pakubwa msiba wa Wanasagamoyo. Thibitisha kwa hoja zozote kumi. (Alama 10).

SEHEMU B: RIWAYA Assumpta Matei: *Chози la Heri*

Jibu swali la 2 au 3

2 ‘...familia yake bado inamiliki mashamba ya michai na mibuni pamoja na mashirika mengi...’

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Kwa kurejelea mifano **minane**, eleza umuhimu wa msemaji katika kujenga riwaya hii. (alama 8)

(c) Jadili kwa hoja **nane** suala la ukoloni mambo leo lilivyoshugulikiwa katika riwaya. (alama 8)

Au

3 Tathmini umuhimu wa mbinu zifuatazo katika kuijenga riwaya ya *Chози la Heri*

Nyimbo (alama 10)

Barua (alama 10)

SEHEMU C: HADITHI FUPI; CHOKOCHO NA D. KAYANDA: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 4 au 5**NDOTO YA MASHAKA**

(4)"...dunia imenikunjulia mikono kunifariji baada ya kunicharaza fimbo yake aushi yangu yote."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
- b) Tambua na ueleze mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo.(al.2)
- c) Eleza jinsi dunia ilimcharaza fimbo msemaji kwa kutolea hoja kumi na nne. (al.14)

AU

(5) Kwa kurejelea hadithi ya Mapenzi ya Kifaurongo, Mame Bakari, Nizikeneni Papa Hapa , Mtihani wa Maisha na Mkubwa, eleza changamoto zinazowakumba vijana. (al.20)

SEHEMU D: USHAIRI**Jibu swali la 6 au 7**

6. SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI. (alama 20)

Pana haja ya kupima, neno tuzowele –angu

Tusizowee kusema , hili ni teuo langu

Huenda huji mapema , -angu huja kuwa tungu

Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu

Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni

Lakini katu si lako, likishavuka menoni

Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani

Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani

Pana haja ya kupima.

Vivyo hivyo kwa lebasi , huwa yako kisutuni

Hivyo nina wasiwasi, wambe yako sebuleni
Itavutiya matusi, ya wenzio insane
Wakakuchoma nafusi, kwa mishale ya lisani
Pana haja ya kupima.

Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele
Lakini katu si wako, nde ukimuletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishilia ni wako, muavye takakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si wako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile
Akupapo akupoko, utaishi palepale
Pana haja ya kupima.

Ni chetu chako si chako, ulimwengu huwa vile
Juhudi zingawa zako, wa kufaidi ni wale
Ikifika siku yako, nyono zikukae mbele
Ulichosema ni chako , huwabakiya wawale
Pana haja ya kupima.

Kaseme na moyo wako , Ubaini haya yale
Ukiambacho ni chako , kisikupe mageule
Kitu utajacho chako , huenda kiwe cha wale

Na usemacho si chako, kiwe chako ndicho kile

Pana haja ya kupima.

MASWALI

- a). Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)
- b) Eleza bahari zozote tatu za shairi hili. (alama 6)
- c) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 4).
- d) Dhihirisha kwa kutoa mifano mitatu matumizi ya uhuru wa mshairi . (alama 3)
- e) Tambua (alama 2)
 - i. Nafsi nenewa
 - ii. Toni
- g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi . (alama 2)
 - Lebasi
 - Punje ukiimezele

au

- 7. SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI. (alama 20)

1. Nikiwa na njaa na matambara mwilini

Nimehudumika kama hayawani

Kupigwa na kutukanwa

Kimya kama kupita kwa shetani

Nafasi ya kupumzika hakuna

Ya kulala hakuna

2. Ya kuwaza hakuna

Basi kwani hili kufanyika

Ni kosa gani lilotendeka

Liloniletea adhabu hii isomalizika ?

3.Ewe mwewe urukaye juu angani

Wajua lilomo mwangu moyoni

Niambie pale mipunga inapopepea

Ikatema miale ya jua

Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?

Je nadhari hujitokeza usoni

Ikielekea huku kizuizini?

Mpenzi mama , nitarudi nyumbani

Nitarudi hata kama ni kifoni

Hata kama maiti imekatikatika

Vipande elfu , elfu kumi

Nitarudi nyumbani

4.Nikipenya kwenye ukuta huu

Nikipitia mwingine kama shetani

Nitarudi mpenzi mama

Hata kama kifoni

Maswali

- a. Taja mambo manne anayoyalalamikia mshairi. (alama 4)
- b. Fafanua dhamira ya shairi hili. (alama 2)
- c. Eleza mbinu nne za kimtindo. (alama 4)
- d. i. Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

ii. Thibitisha jibu la i hapo juu. (alama 4)

e. Tambua katika shairi ; (alama 3)

i. Nafsineni

ii. Nafsi nenewa

iii. Toni

f. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.(alama2)

Hayawani

Nadhari

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI (alama 20)

8

i. Fafanua sifa tano za hekaya. (Alama 5)

ii. Eleza maana ya; (alama 5)

a. Vitanza ndimi.

b. Tahalili

c. Vivugo

d. Matambiko

e. Maapizo

iii. Jadili mifano mitano ya ngomezi za kisasa. (al 5)

iv. Eleza kwa hoja tano udhaifu wa hojaji kama njia ya kukusanya Fasihi Simulizi. (al 5)

MOCK 1

102/3

KISWAHILI FASIHI

KARATASI YA 3

MUHULA WA PILI

MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

a)Jibu maswali manne pekee.

b)Swali la kwanza ni la lazima.

c)Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani Tamthiliya fupi, Ushairi na Riwaya.

d)Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

e)Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	
JUMLA	80	

SWALI 1 LAZIMA SEHEMU YA : FASIHI SIMULIZI

Hapo zamani za kale waliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

MASWALI

- a) Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)
- b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)
- c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)
- d) Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)
- e) Eleza umuhimu wa fomyula:
 - (i) Kutanguliza (al.3)
 - (ii) Kuhitimisha (al.3)

SEHEMU YA B : TAMTHILIA (P.KEA KIGOGO)

Jibu Swali la pili au la tatu.

2 “..... Udongo haubishani na Mfinyanzi. Acha porojo zako. Kigogo hachezewi; watafuta maangamizi!”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
- b) Fafanua mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (al.2)
- c) Eleza sifa zozote nne za msemaji. (al.4)

d)Onyesha ukweli wa kauli hii katika dondoo hili ukirejelea hoja kumi. (al.10)

AU

3.a)Tatizo la uongozi katika bora la Afrika ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kwa kurejelea matukio kwenye Tamthilia ya Kigogo. Jadili ukweli wa kauli hii. (al.10)

b)Eleza mbinu alizotumia Majoka kufanikisha utawala wake. (al.10)

SEHEMU YA C : RIWAYA (A.MATEI : CHOZI LA HERI)

Jibu swali la nne au la tano

4.“Lakini itakuwaje historical injustice, nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b)Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili. (al.4)

c)Fafanua sifa tatu na umuhimu tatu wa msemaji wa maneno haya. (al.6)

d)Taja mambo sita yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho? (al.6)

AU

5.a)”Siasa mbaya maisha mabaya.”Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (al.10).

b)Fafanua athari za umaskini katika jamii ukirejelea Riwaya ya Chozi la Heri.

SEHEMU YA D : HADITHI FUPI (Alifa Chokocho na D.Kayanda (Wahariri)

Jibu swali la sita au la saba.

6.”Lazima niache kazi maana mume wangu haniamini.”

a)Fafanua muktadha wa dondoo hii. (al.4)

b)Eleza sifa sita za mzungumzaji katika dondoo hili. (al.6)

c) Eleza mbinu zifuatazo kama zilivyotumika katika hadithi.

(i) Sadfa (al.6)

(ii) Majazi (al.4)

AU

7. "Hatuwezi kumaliza kula, kila leo tuna kula".

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika. (al.2)

c) Eleza umuhimu wa mnenaji. (al.4)

d) "Lakini nakwambia tena, kula kunatumaliza". Kwa kudokeza hoja kumi jadili ukweli wa kauli hii. (al.10)

SEHEMU YA E : USHAIRI

HEKO JESHI LETU

Hebu niwatangazieni, mitimani yalotanda,
Katu si ya furahani, bali ya mori kupanda,
Kenya yetu I motoni, Al Shabaab katenda,
Katuchokoza yakini, kututeka kama punda,
Lo! Vyombo vya baharini, kwa telki kavidanda.

Wakashambuliya pwani, watalii wakadinda,
Kawapora mifukoni, ilo ndarama mabunda,
Maguruneti jijini, mabomu ja parapanda,
Waasi hawa kidini, kajifunga kwa magwanda,
Wakavuruga amani, ya wakenya waso inda.

Hawa sisi twalaani, kwa usalama kuvunda,
Toka Somalia baini, kuteka Kenya kapenda,
Ndo kavamiya wageni, kisha nao wakaenda,
Kawatesa matekani, kuwafunga kwa mikanda,
Sote kajawa huzuni, kutendewa kama kinda.

Wanajeshi wa nchini, chonjo pasi kusarenda,
Wakenda hivyo vitani, nyoyo bila kuwatunda,
Ka'nzisha operesheni, ya jeshi nchi kulinda
Kajitoma mipakani, huku vikosi meunda,
Somalia sadikini, kawa wa kondo ukanda.

Kwa silaha mikononi, mahandakiyo karanda,
Vita vya anga, jangwani, kulo maji na migunda,
A'Shabab nuksani, kamegwa mfano tunda,
Chao kawa hatarini, wanajeshi kawawinda,
Mchana piya jioni, ngomezi zao kaganda.

Wanamgambo sikieni, kazingirwa kikandanda,
Kavunjavunjwa usoni, miguuni piya vyanda,
Kahasiriwa mwilini, huku kabaki mepinda,
Haramia kawa duni, wakangamizwe manunda
Jeshi kajitahidini, matunda mema katunda.

Habari ulimwenguni, kamoma propaganda,
Kuenezeka kampeni, nazo nchi kama Rwanda,
Jeshi kajitoleeni, siku kadha' za kalenda,
Jeshi letu shukurani, kutulinda ja makinda,
Twakusihi E Manani, tujali kwa kutupenda.

MASWALI

- a)Pendekeza kichwa kingine kinachofaa shairi hili. (al.1)
- b)Onyesha toni ya shairi hili. (al.1)
- c)Eleza nafsi neni katika shairi hili (alama 1)
- c)Ni madhila gani yametendwa na Al Shabab? (al.6)
- d)Fafanua uhuru wa kishairi uliotumiwa na mtunzi katika ubeti wa pili. (al.4)
- e)Eleza muundo wa shairi hili. (al.4)
- f)Eleza maana ya maneno haya yalivyotumwa na msanii. (al.3)
 - i)Magwanda.
 - ii)Mahandaki
 - iii)Maharamia

POST MOCK 1

JINA _____ USAJILI _____ DARASA _____

102/3

KISWAHILI

Karatasiya3

FASIHI

MACHI 2020

MUDA: SAA 2 ½

KCSE POST MOCK 1

Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

Maagizo

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Jibu maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia yaani Kigogo, TumboLisiloshiba ,Ushairi na FasihiSimulizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
5	20	

6	20	
7	20	

SEHEMU A: TAMTHILIA

P. Kea: *Kigogo*

1. Lazima

Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali.

(a) Utaiondoa karaha,

Usiwe kama juha,

Kujipa bure usheha,

Kutembea kwa madaha,

Eti waenda kwa staha,

Ndani kwa ndani kuhaha,

Domo mbele kama mbweha.

Dume acha mzaha,

Shika lako silaha,

Kujipa mwenyewe raha,

Iwe yako shabaha.

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Taja mtindo huu wa uandishi. (alama 1)

(iii) Bainisha tamathali **moja** ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

(iv) Fafanua majukumu ya nafsineni katika tamthilia *Kigogo*. (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika mbalimbali katika tamthilia *Kigogo*. Eleza jinsi mwandishi alivyofanikiwa kutumia nyimbo kuendeleza maudhui, (alama 10)

SEHEMU B: RIWAYA (CHOZI LA HERI)

Jibu swali la 2 au 3

2. “Kumbe hata mja akafanikiwa vipi kielimu na kitaaluma, maisha yake huwa ombwe bila mwana, awe wa kuzaa au wa kulea?”

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Taja tamathali moja iliotumika katika dondoo (alama 1)
- (c) Onyesha ukweli wa kauli hii ukirejelea wahasika wowote **watano** riwayani (alama 5)
- (d) Fafanua umuhimu wa elimu katika jamii ukirejelea riwaya nzima. (alama 10)
3. “Una bahati kupata mfadhili, mimi mzazi wangu wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki na baada ya ule mzozo... biashara imepigwa na mawimbi makali.”
- (a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
- (b) Jadili jinsi mwandishi alivyoshughulikia maudhui ya ufadhili. (alama 6)
- (c) Ukirejelea hadithi zozote tano riwayani, onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya hadithi ndani ya hadithi kujenga maudhui.(alama 10)

SEHEMU C: USHAIRI

Jibu swali 4 au 5

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofautana.

SIONDOKI

- | | |
|------------------------------|--------------------------------|
| 1. | Marungu na bunduki, siondoki. |
| Eti | 3. |
| Niondoke! | Hapa |
| Mimi niondoke hapa | Siondoki |
| Niondoke hapa kwangu! | Mimi nipahame! |
| Nimesaki; licha ya risasi | Niondoke hapa kwangu! |
| Vitisho na mauaji, siondoki. | Fujo na ghasia zikizuka |
| 2. | Na kani ya waporaji, siondoki. |
| Mimi | 4. |
| Siondoki | Haki |
| Niondoke hapa kwangu! | Siondoki |
| Kwa mateke hata na mikuki | Kwangu siondoki |

Niondoke hapa kwangu!
 Nawaje; waje wanaokuja
 Mabepari wadhalimu, siondoki.

5.

Kamwe
 Siondoki
 Ng’oo hapa kwangu!
 Katizame chini mti ule!
 Walizikwa babu zangu, siondoki.

6.

Sendi
 Nende wapi?
 Si’hapa kitovu changu!

MASWALI

- (a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
- (b) Fafanua sifa mbili za nafsineni (alama 2)
- (c) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
- (d) Eleza umuhimu wa kihisishi katika shairi (alama 2)
- (e) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia usambamba katika shairi (alama 2)
- (f) Ukirejelea shairi, eleza namna mtunzi alivyotumia idhini zifuatazo (alama 3)
 - i) Inkisari
 - ii) Kufinyanga lugha
 - iii) Udondoshaji wa neno
- (g) Taja mbinu tatu za lugha katika shairi (alama 3)
- (h) Toa mfano mmoja mmoja wa mishororo ifuatayo (alama 2)
 - i) mshororo mshata

Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi

Si kwamba hapa si kwangu, siondoki.

7.

Katu
 Siondoki
 Sihitaji karatasi
 Niondoke hapa kwangu
 Yangu mimi ni ardhi hii
 Wala si makaratasi, siondoki.

ii) mshororo kifu

5. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

SHAIRI LA A

Faula ngalijua, singalikuwa kijana,
Kwa sababu sikujua, kajipata mvulala,
Mengi mambo nikajua, nikashinda wasichana,
Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Mwili wangu kabadilli, toto hadi utu uzima,
Sauti yangu kabadili, nikajiola mzima,
Kakiuka maadili, dunia nikaizima,
Kweli ujana moshi, ukienda haurudi.

Masikiongu katonga, herini nikavalia,
Nywele yangu nikasonga, na mikufu kuvalia,
Video pia runinga, tazama bila tulia,
Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Malaika kapata, moyo wangu kapambika,
Jina lake kaloreta, mie wangu malaika,

Penzi langu kalipata,mambo mengi katendeka,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Moyongu kausumbua, nilipomtia mboni,

Penzi lanisumbua, aingiapo moyoni,

Sautiye kazindua, yatoa nyoka pangoni,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Penzi lake kalionja, kwangu likawa asali,

Nikawa kionjaonja, kuliwasha kawa kali,

Vitabungu nikakunja, navyo kavitupa mbali,

Kweli ujana ni moshi , ukienda haurudi.

Mzigo kabebesha, ukamwachisha skuli,

Mashakani kaniingisha, nikawa sasa silali,

Kulisaka suluhisho, likawa sasa ghali,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

SHAIRI LA B

Mhariri nipe fursa, nifichue jambo hili,

Nipige wengi msasa, nakusihi tafadhali,

Ukweli wajue sasa, wamakinike ki hali,
Samaki pale barini,kweli huwa si mmoja.

Nawajuza mahawara, pale walipo hakika,
Si ya neni kijasira, ukweli nautamka,
Wayaepeke madhara, wazidi kumakinika
Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Dunia imegeuka, waja leo wana shani,
Wazidi kuhangaika, watatizika moyoni,
Uteshi umeshazuka, mashambani na mijini,
Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Mahaba yakigeuka, hakika huwa ni dhiki,
Ugomvi uje kuzuka, uharibu urafiki,
Wakosane washirika, wapigane kila mwezi,
Samaki pale barini, kweli si mmoja.

Lakini sasa tengeni, vigogo niwasaili,
Iwapo ni hayawani,mpungufu kiakili,
Unisamehe sabini, kwa kosa moja kwa kweli,

Samaki pale barini kweli huwa si mmoja.

Hakika huwa si vyema, kibaya kukimiliki,

Mchongaji nayasema, natangaza uhakika,

Mtu mate huyatema, iwapo hayamezeki,

Samaki pale barini, huwa si mmoja.

Nafumbua fumbo wazi, mnielewe vizuri,

Nafasili ya mapenzi, yalokumbwa nazo zari,

Yalofitinika wazi, hapo ndipo nashauri,

Samaki pale barini, huwa si mmoja.

Maswali

a) Jadili maudhui katika shairi A na shairi B (Alama 6)

b) Eleza muundo wa shairi la A (Alama 4)

c) Toa mifano ya uhuru wa utunzi uliotumiwa katika shairi la B. (Alama 2)

d) Andika ubeti wa nne wa shairi la A katika lugha nathari. (Alama 4)

e) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika mashairi haya. (Alama 4)

i) Nikajiola

ii) Mzigo kambebesha

iii)Shani

iv) Zari

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

6. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

(a) **A:** Kumbe mambo yenyewe rahisi hivi?

B: Rahisi, lakini usije ukabakwa tena

A: Hapana, safari hii itakuwa zamu yako. (*Alimrudishia ... huku akichekacheka*)

C: Hapajaharibika mambo mama'ngu. Kwani la ajabu lipi? Sasa miye namsubiri Bakari mpya tu, hichi kikongwe nikipe talaka. (*Akitabasamu*)

D: Haachwi mtu hapa. Tutabanana humo humo. Yeye atakuwa mke mdogo na mimi mkubwa.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. (alama 2)

(iii) Eleza manufaa saba ambayo jamii hunufaika nayo kwa kushiriki katika kipera hiki. (alama 7)

(b) Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali.

Siwezi kuhutubu. Mimi sikuwafundisha ubaguzi. Kwa nini mnabaguana? Kwa nini hamukuwapa watu wa matabaka yote nafasi ya kuzungumza? Kwa nini? Kwa nini mnafanya hali hii ya kuwa kuna watu na nusu watu? Nataka wazungumze wale ambao hawata sifu tu.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 2)

(ii) Eleza mitindo mitatu katika kifungu hiki. (alama 3)

(iii) Eleza majukumu matano ya kipera hiki katika jamii. (alama 5)

SEHEMU E: HADITHI FUPI

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

“Tulipokutana Tena” (Alifa Chokocho)

5 (a) Halikuwa jambo la kawaida maana maji yalikuwa hayapatikani karibu pale kijijini petu. Sharti mtu aende masafa marefu kuyatafuta. Na sabuni? Sabuni ilikuwa kitu cha anasa kwa familia yetu. Wazazi wangu hakuwa na uwezo wa kununua Sabuni. Labda mara moja moja siku za sikukuu.

(i) Eleza muktatha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Eleza majukumu mawili ya **takriri** katika dondoo hili. (alama2)

(iii) Kwa kurejelea hadithi *Tulipokutana Tena* jadili jinsi haki za watoto zinavyokiukwa. (alama 6)

(b) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa ukirejelea hadithi zifuatazo: (alama 10)

(i) Masharti ya Kisasa

(ii) Ndoto ya Mashaka